

S.L.P 146,

MAGU.

TAREHE: \_\_\_\_\_.

KUMB. NA. LSS/ADM/

JINA LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_

S.L.P \_\_\_\_\_.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUTALE WILAYA YA MAGU MKOA WA MWANZA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Lutale ipo umbali wa kilomita 40 magharibi kutoka Halmashauri ya Magu. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021, mwisho wa kuripoti ni tarehe \_\_\_\_\_ ndani ya siku saba.

**AINA YA SHULE**

Shule yetu ni ya mchanganyiko (Co-Education), ni shule ya kutwa na mwanafunzi anatakiwa afike shule 1:00 Asubuhi. Masomo huanza saa mbili kamili asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri.

**MASOMO YAFUNDISHWAYO SHULENI NA LUGHA YA KUFUNDISHIA**

Tunafundisha masomo rasmi 9 ambayo ni: KIINGEREZA, KISWAHILI, URAIA, HISTORIA, JIOGRAFIA, BAOLOJIA, KEMIA, FIZIKIA, HISABATI na FASIHI YA KIINGEREZA. Masomo yote haya hufundishwa kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne kwa lugha ya Kiingereza isipokua kwa somo la Kiswahili tu. Somo la FASIHI YA KIINGEREZA hufundishwa kuanzia Kidato cha Tatu.

**MTIHANI WA KIPIMO NA ENGLISH ORIENTATION COURSE**

Kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, kila mwanafunzi atasoma kwa wiki sita za kwanza kozi maalumu ya somo la Kiingereza, masomo mengine hayatafundishwa kwa kipindi hiki. Kozi hii inalenga kumpatia mwanafunzi wa kidato cha Kwanza msingi imara wa Lugha ya Kiingereza.

Mwanafunzi awapo shuleni hata ruhuswa kuzungumza Lugha yoyote ile isipokua Kiingereza. Hatua kali huchukuliwa kwa wanafunzi wanaoongea Lugha nyingine tofauti na Kiingereza. Hii inalenga kuimarisha uwezo wa mwanafunzi kuimudu lugha ya kufundishia yaani Kiingereza. Baada ya muda huo wa wiki sita kukamilika mwanafunzi atapewa jaribio maalumu (Aptitude Test), matokeo yake yatakuwa kwa matumizi ya shule.

**2.0 SARE ZETU**

**A. WAVULANA**

- Suruali rangi ya damu ya mzee.
- Mashati meupe mikono mifupi mawili.
- Viatu vyeusi vya kawaida jozi mbili (Sio buti).

- Soksi nyeupe jozi mbili aina ya Stocking.
- Mkanda mweusi usizidi sentimita tano (SM).

**NB:** Suruali zinazotakiwa ni pana na sio modo, ukija umeshona suruali ya aina hiyo hutapokelewa shuleni.

#### **B. WASICHANA**

- Sketi ya rangi ya damu ya mzee yenye michirizi mieupe miwili jozi mbili, marinda yasiozidi sentimita 3.
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vyenye kisigino kisichozi sm 2.
- Jozi mbili za soksi nyeupe aina ya Stocking.

**NB:** Sketi iwe ndefu na iguse kwenye kifundo cha miguu au sentimita kumi kutoka kwenye unyayo wa miguu.

### **3.0 VIFAA VYA DARASANI**

Mwanao anatakiwa aje na vifaa vifuatavyo:-

- i. Madaftari makubwa (Counter Books) yasiopungua tisa (9).
- ii. Kalamu ya Bluu au Nyeusi, penseli na Rula.
- iii. Mathematical Set (Mkebe wa Hesabu).

- Shule ni mahali pa kupata malezi bora na taaluma. Tunasisitiza utii. Wanafunzi wote wanatakiwa kutii sheria, kanuni na taratibu zote za Shule. Pamoja na barua hii pokea nakala ya kiambatanisho kihusucho sheria hizi.
- Endapo mwanao atavunja sheria, taratibu au kanuni hizi mara kwa mara mzazi utalazimika kufika shuleni kusaidiana na walimu kumrudi mwanao.
- Endapo utaratibu wa kawaida wa kumrudi mwanao utashindwa kuleta mabadiliko katika tabia yake, bodi ya shule itahusishwa kutoa maamuzi ya mwisho.

#### **MWISHO**

- Mzazi au mlezi unaombwa kushirikiana na walimu kuifanya Shule ya Sekondari Lutale iwe bora na imara.
- Hudhuria vikao vya wazazi na walimu pale kikao kiitishwapo, changia mawazo ya kuiboresha shule ya mwanao.
- Unashauriwa kumnunulia mwanao mavazi ya michezo kama vile bukta, viatu vya raba n.k.
- Unashauriwa kufika shuleni mara kwa mara ili kujua tabia au mwenendo wa mwanao.

#### **KAMA MWANAO NI MSICHANA**

- Usimwache huru bila mipaka.
- Fuatilia mwenendo wake ili akamilishe elimu yake.
- Mpatie mahitaji ya msingi ili aepuke vishawishi.
- Baba na mama muwe karibu naye.
- Kumbuka walimu pamoja na wazazi wana jukumu moja la malezi kwa mtoto (Mwanafunzi), mlezi ashirikiane na walimu katika malezi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA LUTALE SEKONDARI**

Happiness G. Youze.  
Mkuu wa Shule  
0756230818

#### 4.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa ka mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kuwahi katika shughuli za shule na zingine utakazopewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- h) Kutunza mali za umma.

#### 5.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- a. Wizi
- b. Uasherati na ushoga
- c. Ubakaji
- d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
- e. Kupigana au kupiga
- f. Kuharibu kwa maksudi mali ya umma
- g. Kudharau bendera ya Taifa
- h. Kuwa mjamzito au kupata mimba
- i. Kuoja au kuolewa
- j. Kutoa mimba
- k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l. Kukataa adhabu kwa maksudi
- m. Kuwa na simu ya mkononi

#### 6.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- A. Medical Examination Form ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- B. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A:

FROM THE HEADMISTRESS OF LUTALE SECONDARY SCHOOL DISGNATION

TO THE MEDICAL OFFICER..... (MINISRTY)

.....(DIVISION)

.....(STATION)

MR/MRS/MISS

..... please examine the above named as to his/her fitness for further studies please (insert title of post on temporary contract permanent and pensionable terms).

Date..... Signature.....

PART B: (MEDICAL CERTIFICATE)

I have examined the above and consider that he she is physically fit for further studies as a student.

.....  
.....  
.....  
.....

DATE..... SIGNATURE.....

STATION.....DESIGNATION.....

## FOMU YA MAELEZO JUU YA MWANAFUNZI

1. Jina..... (hili liwe ulilotumia shule ya msingi na utatakiwa ulitumie miaka yote)
2. Dini: .....
3. Tarehe ya kuzaliwa: .....
4. Shule uliyotoka: .....
5. Michezo uipendayo au shughuli uzipendazo: .....
6. Unaishi na nani: .....
7. Jina la baba au mlezi: .....
8. Kazi ya baba au mlezi: .....
9. Mahali ambapo baba au mlezi anapoishi: .....

Pamoja na barua hii yafuatayo ni muhimu uyasome na kuyaelewa alafu mwanao ajaze fomu zinazotakiwa kujazwa ndipo aje shuleni na barua hii pamoja na mambo yatakiwayo kama ifuatavyo:

1. Sheria za shule- uzisoe na kuzielewa pamoja na mwanao
2. Fomu ya mwanafunzi-ijazwe na mwanafunzi mwenyewe
3. Cheti cha hospitali-hii lazima mwanao apimwe katika hospitali ya serikali ili hali yake ya kiafyaiweze kueleweka. Ijazwe Medical Examination Form na kukabidhi shuleni.

Kukiri kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule:

Mimi: .....Mzazi/Mlezi pamoja na mwanangu  
..... (Mwanafunzi) tumezisoma, tumezielewa na kwa kuwa  
mwanafunzi atazifuata na kuzitii, kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Jina la mzazi au mlezi.....Sahihi.....

Jina la mwanafunzi.....Sahihi.....